



JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI WA MBULU

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Simu 255 271 2533331
Barua pepe: td@mbulutc.go.tz

S.L. P 164,
MBULU-MANYARA

Kumb. Na. MTC/TD/FI/19/10

25/05/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Mji wa Mbulu inatangaza nafasi za kazi kama ifuatavyo:

1. MTENDAJI WA KIJIKI (nafasi 24)

SIFA ZA MWOMBAJI

Awe na Elimu ya Kidato cha nne (form IV) au sita (Form VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/cheti katika moja ya fani za Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU:

- i) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali za Kijiji/Mtaa.
- ii) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji/Mtaa.
- iii) Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya Maendeleo ya Kijiji/Mtaa.
- iv) Katibu wa Mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji/Mtaa.
- v) Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi) Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na mkakati wa kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii) Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya kitaalamu katika Kijiji/Mtaa.
- viii) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji/Mtaa.
- ix) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- x) Kuandaa na kutunza rejesta ya wakati wote wa Kijiji/Mtaa.
- xi) Kusimamia utungaji na utekelezaji wa sheria ndogo za Kijiji/Mtaa.
- xii) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

MSHAHARA:

Mshahara utalipwa kwa kuzingatia viwango vya serikali kuanzia TGS B/1.

2. DEREVA DARAJA LA II – TGS B (nafasi 2)

SIFA ZA MWOMBAJI

Awe na cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na leseni ya daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka bila kusababisha ajali.


MAJUKUMU YA KAZI

- i) Kukagua gari kabla ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- ii) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- iii) Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
- iv) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- v) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- vi) Kufanya usafi wa gari.
- vii) Kufanya kazi nyingine kadri anavyoelekeza na msimamizi wake.

3. MAELEKEZO KWA WAOMBAJI:

- a) Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenye umri kati ya miaka 18 na usiozidi 45.
- b) Maombi yaambatishwe na taarifa ya maelezo binafsi (Curriculum Vitae) ya muombaji ikionesha wadhamini watatu na taarifa zao sahihi namba za simu za muombaji na wadhamini, cheti cha taaluma, cheti cha Kidato cha Nne, cheti cha kuzaliwa na picha mbili passport size (ziandikwe majina kwa nyuma).
- c) Testimonial na Provisional Statement of Results hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na cha Sita havitapokelewa.
- d) Waombaji waliostaafu/kustaafishwa au kuacha kazi katika Utumishi wa umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kwa kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- e) Muombaji atakayewasilisha taarifa za kughushi atachukuliwa hatua za kisheria kwa mujibu wa taratibu.
- f) Barua zote ziandikwe kwa mkono kwa lugha ya Kiswahili au kiingereza.
- g) Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
- h) Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatanishe cheti cha ulinganifu (Equivalent Certificate) kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania.
- i) Kwa waombaji wenye vyeti vya ngazi ya NTA level 4 "Basic Technician Certificate" (NTA level 4) maombi yao hayatafanyiwa kazi kwa sasa cheti kinachopokelewa ni Technician Certificate (NTA level 5) na kuendelea.
- j) Maombi yatumwe kwa njia ya posta kwa kutumia anwani Mkurugenzi wa Mji, S.L.P. 164, Mbulu au yawasilishwe kwa mkono siku za kazi Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji kabla au ifikapo tarehe 10/06/2022 saa 9.30 jioni.
- k) Watakaochaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili pia kupitia tovuti ya Halmashauri www.mbulutc.go.tz pamoja na mbao za matangazo na kupitia simu zao za mkononi.

4. Tangazo hili ni marekebisho ya tangazo la tarehe 24/05/2022.


Yefred Myerzi

Mkurugenzi wa Mji

HALMASHAURI YA MJI WA MBULU